MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.14: Msimu wa Kilimo 2025/26* *Tathmini ya Februari 11 -20, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Februari 21-28, 2026*



**MUHTASARI**

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, zitasaidia katika ukuaji wa mazao.
- Hali ya vipindi vya mvua nyepesi inayotarajiwa katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka zitasaidia katika uandaaji wa mashamba kwa ajili ya msimu wa kilimo wa Masika.
- Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kushirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao huku wakiendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2026

Katika kipindi hiki cha dikadi, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupunguza nguvu wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi yetu, nyanda za juu kusini magharibi na kusini, Kanda ya kati na kusini mwa nchi. Aidha, uwepo wa Kimbunga "GEZANI" katika eneo la rasi ya Msumbiji uliimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo ya kusini mwa nchi ikiwa ni pamoja na pwani ya kusini, hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea uwepo wa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, Kati, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi, ukanda wote wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2026

Katika dekadi hii, maeneo mengi nchini yalipata kiasi cha mvua katika siku kumi cha kati ya milimita 26 hadi 200. Hata hivyo, baadhi ya maeneo katika Nyanda za Juu kusini magharibi, hususan mikoa ya Ruvuma, Njombe na kusini mwa Iringa, yalipata kiwango cha juu zaidi cha mvua kilichokuwa kati ya milimita 100 hadi 150 kwa siku kumi. Wakati huo, maeneo mengi ya mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam na Pwani, pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba, yalipata kiasi cha mvua kilichokuwa chini ya milimita 25, kama inavyoonekana katika Kielelezo cha 1.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Februari 11-20, 2026

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2026

Katika dekadi hii, mvua zilizonyesha katika maeneo mengi ya nchi zilipelekea kuongezeka kwa unyevunyevu wa udongo na hivyo kusaidia ukuaji wa mazao. Hata hivyo, katika mkoa wa Kagera, mvua hizi ziliathiri vibaya mazao yaliyokuwa bado yako mashambani yakisubiri kuvunwa.

Katika maeneo yanayopata mvua za misimu miwili, hususan ukanda wa pwani ya kaskazini, zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya ukomavu. Hata hivyo, hali ya ukavu iliathiri ukuaji wa zao la mahindi katika maeneo mengi. Katika bonde la Ziwa Victoria (Kagera na Mwanza) pamoja na nyanda za Juu za kaskazini mashariki (Kilimanjaro, hasa wilaya ya Rombo), wakulima waliendelea na shughuli za uvunaji wa mahindi. Wakati huo huo, katika mkoa wa Morogoro, zao la mpunga lilikuwa katika hatua ya ukuaji wa majani.

Kwa maeneo mengi yanayopata mvua za msimu mmoja, zao la mahindi kwa ujumla lilikuwa katika hatua ya ukuaji wa majani, isipokuwa katika mkoa wa Tabora ambako mahindi yalikuwa katika hatua ya ukomavu wa nta. Aidha, katika

maeneo mengi ya mkoa wa Dodoma, mazao ya alizeti na mtama yalikuwa katika hatua ya kuota.

Kwa mazao ya kudumu, kahawa ilikuwa katika hatua ya kutunga matunda, hususan katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe.

Upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo na wanyamapori uliimarika katika baadhi ya maeneo ya nchi kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2026

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kiliongezeka kiasi hususan kwa maeneo ambayo yaliyokuwa na ongezeko la mvua.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudumisha uwepo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) katika maeneo ya magharibi mwa nchi yetu, Kanda ya Zwiwa Victoria, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupelekea Kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2026

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajia kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajia kupata vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), nyanda za juu kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), Kanda ya kusini, Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajia kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2026

Hali ya mvua inayotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka itaongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji wa mazao.

**Ushauri:**

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (kanda ya ziwa Victoria, Pwani ya Kaskazini na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki):** Hali ya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi inayotarajiwa zitasaidia katika shughuli za uandaaji wa mashamba kwa msimu wa kilimo wa Masika unaotarajiwa**.** Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua (nyanda za juu kusini magharibi, mikoa ya magharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya kusini):** Mvua zinazotarajiwa katika maeneo haya zitasaidia ukuaji wa mazao. Wakulima wanashauriwa kufuatlia hali ya mazao na pia kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku.
- **Malisho na upatikanaji wa maji kwa wafugaji:** Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya malisho na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- **Wavuvi wa Samaki baharini na maziwa makuu:** Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kujua wakati sahihi wa kufanya shughuli za uvuvi kutokana na uwezekano wa kujitokeza mawimbi makubwa na upepo mkali

Ushauri huu umedhamiria kuongeza tija kwenye kilimo na kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya Hewa. Wadau wote wa kilimo wanahimizwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa ili kuwa na mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2026

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kudumishwa kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)